



KARATASI YA UKWELI

MAREKEBISHO YA MAKOSA YA JINAI (UKEKETAJI WA WANAWAKE) SHERIA YA 2013

Sheria ya zamani

Zamani, chini ya kipengere cha 186C cha Makosa ya Jinai, ilikuwa kosa la jinai kwa mtu kutoa mtoto kutoka Mkoa wa Kaskazini, au kufanya utaratibu wa kufanya hivyo, kwa lengo la kufanya ukeketaji wa wanawake. Hata hivyo, haikuwa kosa kupanga kuondoa mtu mzima kutoka Mkoa wa Kaskazini kwa lengo hilo hilo.

Je sheria mpya inafanya nini?

Marekebisho ya Makosa ya Jinai (Ukeketaji wa Wanawake) Sheria ya 2013 iliyoanza 4 Desemba 2013.

Sheria inarekebisha kipengere cha 186C cha Makosa ya Jinai ili itumike kwa wate wanawake na watoto. Hii ina maana kuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumchukua mwanamke, awe ni mtu mzima au mtoto, kutoka Mkoa wa Kaskazini, au kufanya utaratibu wa kufanya hivyo, kwa lengo la kufanya ukeketaji wa wanawake.

Sheria hii haina nia ya kuwaadhibu au kuwashtaki wahusika. Matokeo yake, hata kama huyo mwanamke akikubali kuweza kuondolewa kutoka Mkoa wa Kaskazini, hataweza kushtakiwa kwa kosa hilo. Madhumuni ya kosa ni kuadhibu tu vitendo vya watu wengine ambao huondoa au kufanya mipango ya kuondoa wanawake kutoka Mkoa wa Kaskazini, kwa nia ya kufanya ukeketaji.

Kwa nini sheria ilibadirika ?

Katika mwezi Machi 2013 ripoti ya kitaifa ijulikanayo kama Mapitio ya Mfumo wa Ukeketaji ya Australia iliweza kuchapishwa. Ripoti ilitoa idadi kubwa ya mapendekezo kuhakikisha kunakuwepo ulinzi mkubwa kwa wanawake na watoto kutokana na ukeketaji. Mwezi Aprili 2013 Mkoa wa Kaskazini ulikubali kuchukua hatua ili kuweka katika vitendo mapendekezo ya ripoti. Sheria Mkoa wa Kaskazini tayari ilitoa ulinzi kwa mujibu wa mapendekezo makubwa ya ripoti hiyo, hata hivyo, ulinzi wa mtu kutoweza kuondolewa kwenda nchi nyingine au mkoa kwa lengo la ukeketaji wa wanawake ulikuwa tu unalenga watoto bila kujumuisha wanawake wakubwa. Hakuna sababu za kubana watoto tu kuweza kuondolewa zilizoweza kuonekana.

Matokeo yake, aina ya kosa imeweza kubadilishwa ili kuhakikisha kuwa wanawake na watoto wote wanalindwa kutokana na kuondolewa kwenda mkoa au nchi nyingine kwa lengo la kufanyiwa ukeketaji wa uke.

Adhabu

Kama mtu akimtoa mwanamke, awe mtu mkubwa au mtoto, kutoka Mkoa wa Kaskazini, au kufanya mipango ya kufanya hivyo, kwa lengo la kufanya ukeketaji wa mwanamke, atakuwa amefanya kosa la jinai. Mtu huyo anaweza kufungwa kifungo mpaka cha miaka 14 jela.

Ni lini sheria mpya itanza kufanya kazi ?

Mtu yeyote atakayemtoa mwanamke kutoka Mkoa wa Kaskazini, au kufanya mpangilio wa kufanya hivyo, kwa lengo la kufanya ukeketaji wa mwanamke kuanzia 4 Desemba 2013 atakuwa amefanya kosa la jinai. Hata hivyo, kama kosa lilifanyika kabla ya tarehe 4 Desemba 2013, basi wakosaji wanaweza kuadhibiwa tu kama waliondoa au kufanya mpango wa kuondoa mtoto kutoka Mkoa wa Kaskazini kwa lengo la kufanya ukeketaji wa mwanamke.